

Vyombo vya habari nchini Kenya na kwingine ulimwengu hutokeleza jukumu muhimu katika kupasha umma habari za ugaidi. Uteuzi wa lugha katika kuripoti habari hizi ni muhimu katika kuwasilisha habari. Hata hivyo uteuzi wa lugha unaweza na athari mbalimbali kwa wasomaji wa habari za ugaidi. Hali hii inaweza kusababisha uadui, kutuamini ana na mielekeo hasi kuhusu baadhi ya watu katika jamii na hata dini. Utafiti huu umechanganua matini za ugaidi wa kitafita na kimataifa katika gazeti la *Taifa Leo* linalochapishwa nchini Kenya. Lengo la utafiti lilikuwa kuchanganua usemi unaotumiwa kuripoti habari za ugaidi katika gazeti hili. Madhumuni mahsusi ni kuchunguza vipengele vya lugha vilivyotumiwa kuwasilisha habari za ugaidi; kama uteuzi huo wa lugha ulikuwa na ishara za mwegemeo; kuhakiki athari ya habari hizo kwa wasomaji na kuchunguza namna sera ya uhariri ilivyoathiri uteuzi wa lugha. Nadharia Hakiki ya Uchanganuzi Usemi kama ilivyofataniwa na Teun van Dijk (1988), Norman Fairclough (1989) na Ruth Wodak (2001) imetumiwa. Muundo wa utafiti ni mseto wa Kipekuzi na Kimaelezo. Magazeti ya *Taifa Leo* yaliyochapishwa kati ya Oktoba 2010 hadi Novemba 2011 yamechunguzwa. Uchukaji wa sampuli dhambiwa ambapo magazeti yenye taarifa za ugaidi ndiyo yaliteuliwa na kuchunguzwa. Maoni ya wasomaji yamekusanywa na kuchunguzwa kuhusu habari za ugaidi walizopokea. Jumla ya wasomaji 419 walishirikishwa katika uchunguzi. Waliteuliwa kishalabeta kutoka miji mime-Mombasa, Nairobi, Nakuru na Muias ambayo ina wasomaji wengi zaidi wa gazeti hili. Miji hiyo inawakilisha maeneo ya Pwani, Kati, Bonde la Ufa na Magharibi nchini Kenya. Waandishi wa habari wanaoshughulikia habari za ugaidi nao walihojiwa. Waandishi hao wa habari waliteuliwa kimatlababa. Wale wote ambao hushughulikia habari za ugaidi walishirikishwa. Data ya kithamano imechanganuliwa kwa kuchunguza mawasiliano, maoni na majibu ya wasomaji. Data ya kiwingitidadi imewasilishwa katika majedwali na asilimia ili kuonyesha walioathirika na habari za ugaidi. Utafiti uligundua kwamba lugha inayotumiwa kuandika habari za ugaidi ina ishara za mwegemeo. Mwegemeo huo una athari hasi miongoni mwa wasomaji. Pia ilibainika kuwa mizozo hutokea kutokana na habari za ugaidi zilizosomwa kwenye gazeti hili. Vilevile kulikuwa na hali ya kushukiana miongoni mwa wasomaji kutokana na habari hizi. Sera ya kampuni ya Naton Media nazo ziligunduliwa zinachangia katika uteuzi wa lugha inayogemeza habari za ugaidi zinazochapishwa katika gazeti la *Taifa Leo*. Utafiti huu umengazia haja ya kutanua makini katika uteuzi wa lugha; vyanzo vya habari na nafasi ya uwasilishaji wa usemi katika kuripoti habari za ugaidi ili kupunguza mwegemeo na athari hasi zinazosababishwa na mwegemeo huo. Unaweza pia kuchangia katika kuibua mtazamo utao kuhusiana na ugaidi na kwa hivyo kuchangia katika dhidi ya ugaidi. Ufahamu wa kutosha kuhusiana na swala la ugaidi ni hatua muhimu katika kupambana na ugaidi pamoja na athari zake.